MEDIA COUNCIL OF KENYA

# Kanuni za utendakazi wa uanahabari nchini Kenya

## Jedwali la Pili la Sheria ya Baraza la Habari la 2013

# Jedwali la Yaliyomo


Usahihi na uzingatiaji haki ........ 5

Uhuru ........ 6

Uadilifu ........ 7

Uwajibikaji ........ 9

Haki ya kujibu tuhuma - haki ya kujitetea ........ 9

Vyanzo vya habari visivyotambuliwa ........ 10

Usiri (kuwalinda vyanzo vya habari kwa kutowafichua) ........ 10

Kutojitambulisha ........ 10

Lugha chafu, matusi, matamshi yanayosikitisha na kuibua hamasa ........ 11

Kulipia habari- mtu kutoa pesa kwa wanahabari au chombo ili habari zichapishwe. ........ 11

Kufuatilia mizozo ya kikabila na kidini ........ 12

Kurekodi mahojiano na mawasiliano ya simu ........ 12

Faragha- Haki za mtu kufanya mambo binafsi ........ 13
Kuingilia majonzi ya watu na mishtuko ........ 14
Jinsia na ubaguzi ........ 14
Uanahabari wa masuala ya fedha ........ 14
Barua kwa mhariri ........ 15
Kulinda watoto ........ 15
Waathiriwa wa dhuluma za kijinsia ........ 16
Kutumia picha na majina ........ 16
Jamaa na marafiki ambao hawajahusika kwenye tukio ........ 17
Matendo ya Vurugu ........ 17
Majukumu ya mhariri ........ 17
Matangazo ya kibiashara ........ 18
Matamshi ya chuki ........ 18

# Utangulizi

Tukiwa taasisi inayoongoza katika kuratibu shughuli za vyombo vya habari ikiwemo kuhakikisha nidhamu ya kikazi miongoni mwa wanahabari nchini Kenya, mojawapo ya majukumu ya Baraza la Vyombo vya habari ni kuhamasisha uwepo wa viwango vya juu vya heshima za kikazi miongoni mwa wanahabari nchini Kenya. Mbali na kuhamasisha na kulinda uhuru na nafasi ya vyombo vya habari kuonyesha mawazo huria kazini mwao, Baraza la Vyombo vya habari pia linalenga kuhakikisha kwamba kanuni za kazi miongoni mwa wanahabari, na vyombo vya habari zinalindwa. Kanuni za utendakazi wa shughuli za uanahabari nchini Kenya zilinakiliwa kwenye ratiba ya pili ya Sheria ya Vyombo vya Habari (2007) na zinaongoza namna ambavyo yeyote anayehusika kwenye uanahabari nchini Kenya anafaa kuendeleza shughuli zake.

# 1 Usahihi na uzingatiaji haki

1. Malengo ya kimsingi ya mwanahabari ni kuandika taarifa ya haki, sahihi na isiyo na upendeleo kuhusu matukio na masuala muhimu machoni pa umma. Kauli zote kulihusu tukio analoangazia mwanahabari au swala zafaa kushirikishwa kwenye taarifa yake kadri ya uwezo wake. Yeyote anayetajwa kwenye tukio au swala kwa njia inayoshusha hadhi yake au heshima zake, anafaa kupewa nafasi ya kujieleza.

2. Punde inapobainika kwamba taarifa isiyo sahihi imechapishwa, taarifa inayowasilisha ujumbe wa uwongo, ichapishwe au ipeperushwe mitamboni, yafaa taarifa ya marekebisho iandaliwe kwa haraka na kuchapishwa au kupeperushwa. Marekebisho yanayoandaliwa yanafaa kuwasilisha usahihi ambao haukuwa kwenye taarifa ya awali. Marekebisho hayo pia yataje kosa lililofanywa kwenye taarifa ya kwanza bila kulirejelea kosa hilo.

3. Kuomba msamaha huchapishwa au ukapeperushwa kuambatana na maagizo ya Baraza la Vyombo vya habari

4. Taarifa zikikosa usahihi na uendelezaji wa haki kwa wahusika basi zisichapishwe. Licha ya kwamba wanahabari wana haki ya kuunga mkono pande fulani, yafaa waoneshe waziwazi kwenye taarifa zao tofauti baina ya hoja, maoni na ukweli wa jambo/tukio

5. Kwa ujumla, vichwa vikuu vya habari magazetini kwenye taarifa za televisheni au rediyo visiwe vya kushtusha. Vichwa vya habari vinafaa kuendana na maelezo yaliyomo kwenye taarifa ile. Vichwa vya habari vinavyotoa madai vyafaa pia kupambanua kwa kumtaja aliyetoa madai hayo au ikiwezekana madai hayo yatiwe alama za nukulu

6. Wanahabari wanapaswa kutangaza habari wakizingatia haki bila kupendelea upande wowote. Suala kuu wanalozingatia ni umuhimu wa taarifa ile kwa umma- kwamba taarifa ile inafaa kupeperushwa wakati fulani na kwamba inaufaa umma kwa njia fulani.

7. Wanahabari wanapaswa kuwachukulia wahusika wote kwenye taarifa wanazokusanya kwa heshima, huku wakionesha upendo kwa waathiriwa wa visa vya uhalifu au majanga ya dharura

8. Wanahabari wanapaswa kila mara kutaka kuelewa na kuzifahamu barabara jamii zilizopo katika eneo wanalofanyia kazi ya uanahabari. Ufahamu huo utawawezesha wanahabari kuripoti masuala kuzihusu jamii hizo bila kuathirika kwa kejeli za kijamii. Utawawezesha kuyashirikisha maoni na hoja kutoka pande zote kwa njia inayofafanua masuala ifaavyo.

9. Wanahabari na washirika wengine katika vyombo vya habari wanapaswa kutangaza au kuchapisha habari kwa njia inayochangiwa na tafakari ya kina wakizigatia mitizamo ya kitaaluma wala sio misimamo binafsi.

## 2 Uhuru

Wanahabari wana wajibu wa kutetea na kulinda uhuru wa uanahabari, uhuru wao wa kuendesha shughuli za uanahabari na uhuru wa wanahabari wenzao kutokana na miingilio ya wale wanaotaka kushawishi namna ambavyo taarifa za habari zinafaa kufanywa. Wanahabari wanapaswa ku;-

1. Kusanya na kuripoti habari bila woga wala mapendeleo huku wakikataa katakata kutii wito wa wale wanaowashiwishi kutoka pande zozote ikiwemo wanaotafuta huduma za matangazo ya

kibiashara, vyanzo vya habari, wahusika kwenye matukio ya habari, watu wenye ushawishi mkubwa, na makundi yenye mahitaji maalum

2. Kukataa wito wa wale wenye nguvu za kisiasa za kushawishi mielekeo ya habari zilizopo au wale wenye nia ya kuwatisha wale wanaohusika kwenye ukusanyaji wa habari na kuzichapisha au kuzitangaza.

3. Kuamua habari ipi ndiyo muhimu kwa kutegemea kanuni za uhariri wala sio kwa kutegemea ushawishi wa makundi kutoka nje

4. Mwanahabari kukataa kushawishiwa na misimamo binafsi au hata misimamo ya wenzake katika fani ile- misimamo inayoweza kuathiri wajibu wa uanahabari na huduma kwa umma.

5. Tambua kwamba ufadhili wa taarifa za habari hautatumiwa na wafadhili kuamua taarifa zipi ndizo muhimu au kuzuia na kushawishi mtizamo wa habari zinazoandaliwa

6. Kukataa wito wa wamiliki wa chombo cha habari au mameneja wa shirika la habari kushawishi namna ambavyo taarifa za habari huandaliwa au huchaguliwa na kuchapishwa au kupeperushwa.

## 3 Uadilifu

Wanahabari wanapaswa kutangaza habari kwa uadilifu na heshima za kikazi huku wakijiepusha na ushawishi kutoka nje unaoweza kuzua mkanganyiko baina ya kazi na shughuli zao binafsi – uanahabari wafaa kufanywa kwa njia inayoonesha kwamba wasomaji watazamaji wasikilizaji n ahata wahusika kwenye matukio ya habari ni watu wenye ufahamu tosha na wanaelewa kosa li wapi. Kwa hivyo wanahabari wanapaswa ku;-

1. Taja vyanzo vya habari kadri inapowekezekana- kwamba habari zilitolewa na nani au zilitoka wapi. Vyanzo vya habari vinapotaka kuchukuliwa kwa usiri na faragha vipewe heshima ile iwapo itafaa machoni pa umma- kwamba kuelezea vyanzo vya habari si muhimu kama habari zenyewe. Vilevile vyanzo vya habari vinaweza kupewa faragha iwapo ni hatua ya kulinda maisha ya aliyetoa habari ile

2. Kila mara, siku zote, tofautisha baina ya hoja maoni na taarifa ya habari – maoni au hoja vitajwe kuwa maoni/hoja

3. Tumia mitambo yenye teknolojia ya kisasa kwa uangalifu, jiepushe na njia za kutumia teknolojia zinazobadilisha uhalisia wa tukio au jambo au kutia chumvi kwenye tukio.

4. Tumia mitambo ya kunasa sauti kwa kisiri au kamera zilizofichwa iwapo umekosa njia nyingine za kukusanya habari. Mbinu hiyo hukubalika tu iwapo hamna njia nyingine au kwamba habari unazokusanaya zina umuhimu mkubwa hivi kwamba namna ambavyo zilikusanywa si hoja muhimu tu ni kwamba habari zimepatikana. Vilevile ni muhimu njia iliyotumika kupata habari hizo itangaziwe wasomaji wasikilizaji na watazamaji.

**Wanahabari hawaruhusiwi ku;**

1. walipa pesa zozote vyanzo vya habari hasa wale wenye nia ya kutoa habari ili wapewe malipo.

2. kubali zawadi, malipo ya namna yoyote au hata kuandaliwa vitamu na wale wenye nia ya kutaka kuangaziwa kwa njia inayowafaa wao.

3. shiriki kwenye shughuli zinazoathiri uhuru wao wa kuzingatia uadilifu kwenye shughuli zao za kikazi na uwezo wa mawazo huria

## 4 Uwajibikaji

Wanahabari na wafanyakazi wote katika sekta ya habari wanapaswa kufahamu kwamba wanawajibikia umma hasa kwenye matendo yao ya uanahabari – vilevile wanawajibikia taaluma ya habari na wao binafsi. Kwa hivyo wanapaswa ku;-

1. Hamasisha kwa moyo wote wanahabari na washirika wengine kwenye vyombo vya habari watii kanuni hizi
2. Itikia wito wa umma kwa kujibu maswali yao, chunguza malalamiko halafu rekebisha makosa yaliyopo tena kwa haraka,
3. Elewa kwamba ukiwa mwanahabari una wajibu wa kuendesha shughuli zako kwa kuzingatia kanuni za utendakazi ya uanahabari

## 5 Haki ya kujibu tuhuma - haki ya kujitetea

Siku zote vyombo vya habari vinapaswa kutoa nafasi kwa watu au mashirika kujieleza iwapo umetokea ukosefu wa usahihi kwenye habari zilizochapishwa. Iwapo ombi la kujieleza limemfikia mhariri kwa njia ya barua, mhariri wa chombo anaidhinishwa kuchapisha barua ile nzima au sehemu ya barua ile tu, hasa iwapo ni barua ndefu. Hata hivyo kiwango anachoamua kuchapisha kinafaa kusheheni msingi wa malalamiko ya aliyetuma barua ile ili iwe jibu dhidi ya madai yaliyomkumba.

## 6 Vyanzo vya habari visivyotambuliwa

Vyanzo vya habari na wote wanaofichua mambo siku zote yafaa watajwe majina yao- kumaanisha kutumia vyanzo vya habari bila kutaja majina ya vyanzo hivyo hakuruhusiwi isipokuwa iwapo juhudi za mwanahabari kutafuta ukweli zinanufaika na kufanikiwa vyema kwa kutowataja wanaotoa habari. Hata hata hivyo ripota wa habari na vilevile mhariri wa chombo anafaa ajue jina la anayetoa habari au vyanzo vyovyote vya habari hizo. Ikitukia kwamba zipo habari zilizotumika kwenye taarifa ya habari ambazo zilitokana mahala tofauti na pale ambapo ripota wa habari alizipata, yafaa chanzo chake au vyanzo vitajwe.

## 7 Usiri (kuwalinda vyanzo vya habari kwa kutowafichua)

Ni hitaji muhimu katika fani ya uanahabari kwamba wanahabari daima wawalinde kwa kutowafichua wale wanaowapa habari muhimu zenye manufaa kwa umma –Usiri!

## 8 Kutojitambulisha

Wanahabari wanapaswa kujitambulisha rasmi wanapotembelea afisi zozote kwenye shughuli zao za kutafuta habari, au kupiga picha iwe za video au za kawaida. Ni kinyume cha kanuni za uanahabari kutafuta habari kwa njia za siri au kupitia kutojitambulisha. Kukusanya habari kupitia njia ya kutojitambulisha kunafaa kutumika katika mazingira ambayo hamna njia nyingine za kupata habari ambazo ni muhimu kwa umma.

## 9 Lugha chafu, matusi, matamshi yanayosikitisha na kuibua hamasa

1. Ni hitaji muhimu katika fani ya habari kwamba wanahabari wasichapishe habari au kutangaza kwa kutumia lugha chafu, matusi au matamshi yanayowakasirisha wasomaji wasikilizaji na watazamaji- iwapo maneno kama hayo yatatumika kwa namna yoyote basi lazima iwe kwamba yanatoa habari muhimu kwa umma

2. Kanuni hii pia inashirikisha picha- kwamba kuchapisha picha za maiti au miili ya watu iliyokatikakatika vibaya, picha za damu ya watu, au mazingira yenye matukio ya kutisha yasionyeshwe watamazamaji. Iwapo picha zinazoonyesha haya zitatumika basi iwe ni kuwasilisha ujumbe muhimu kwa umma.

## 10 Kulipia habari- mtu kutoa pesa kwa wanahabari au chombo ili habari zichapishwe.

Siku zote mtu akutoa pesa kulipia utoaji wa habari Fulani, hali hiyo inaibua shaka kwamba huenda ahabari anazotaka zichapishwe hazina umuhimu kwa umma na kwamba huenda ni habari za uwongo. Yafaa ieleweke malengo ya anayelipia habari hizo ni yapi na anayezipokea pia ana malengo gani. Kwa hivyo iwe kanuni kwamba wanahabari hawatapokea pesa zozote kuwa kichocheo cha kuchapisha habari Fulani.

## 11 Kufuatilia mizozo ya kikabila na kidini

1. Habari, maoni na kauli zozote kuhusu mizozo ya kikabila, kidini au kuhusu tofauti za makundi mbalimbali zinapaswa kuchapishwa tu iwapo zimepigwa msasa ifaavyo ikiwemo kuangalia vyema yote yanayosemwa maana lengo kuu la kuangazia mizozo kama hii ni kupalilia mapatano ya taifa, maelewano na Amani.

2. Vichwa vya habari vya kuwatisha watu au kuwahamasisha kuchukua hatua fulani visitumike.

3. Tarifa za habari au maoni kuhusu maswala Fulani yasichapishwe au kutangazwa kupitia njia inayochochea hamasa, kutia chumvi mizozo, au kuongeza makali ya zogo baina ya jamii. Vilevile taarifa za habari zinazoweza kupalilia mizozo zafaa kuepukwa na wanahabari.

## 12 Kurekodi mahojiano na mawasiliano ya simu

1. Suala la kunasa sauti za wanaohojiwa linaruhusiwa tu iwapo mwanahabari amemjulisha mhusika kwamba ananasa sauti yake- wanahabari hawatanasa watu kwenye video au sauti kabla kupata idhini yao. Licha ya hiyo ipo idhini ya mwanahabari kumnasa mhusika bila idhini yake iwapo suala analoshughulikia mwanahabari ni tete na linaweza kufikishwa kortini- kwa hivyo mwanahabari atahitaji nakala ya kanda kujitetea. Kanuni hii itatumika kwenye vyombo vyote vya habari vikiwemo televisheni na radio

2. Kabla kurekodi mazungumzo ya simu ili itumike kwenye matangazo ya rediyo na televisheni, chombo cha habari kinapaswa kumjulisha

mhusika kwamba kitatumia nakala iliyorekodiwa kwenye matangazo yake. Kanuni hii hata hivyo haitumiki kwenye muktadha ambapo vyombo vya habari huendesha vipindi ambavyo kwa wingi watu hupiga mle simu na inajulikana kwamba chombo hicho cha habari hupeperusha mazungumzo ya simu kila leo.

## 13 Faragha-Haki za mtu kufanya mambo binafsi

1. Haki ya umma kupata habari muhimu zafaa kulinganishwa na haki ya watu maarufu kuendesha mambo yao binafsi kwa faragha. Haki ya umma kupata habari haipaswi kuzidi haki ya watu maarufu kupata nafasi ya kushughulikia mambo yao bila kuingiliwa na vyombo vya habari.

2. Wanahabari wanapaswa, daima, kulenga masuala yenye umuhimu kwa umma wala sio shughuli binafsi za mtu

3. Kuingilia maisha binafsi ya mtu, kuuliza maswali kuhusu maisha hayo, bila idhini ya mtu husika, ni jambo lisilokubalika- idhini yaweza kutolewa kwa wanahabari kufanya hivyo iwapo, maisha binasfi ya mtu maarufu yana umuhimu kwa umma. Mahitaji ya umma pia kuhusu suala kama hili yanafaa yawe yenye umuhimu mkubwa wala sio kutokana na fikra za kupita tu za mwanahabari zinazomshinikiza kuingilia maisha binafsi ya mtu. Masuala yote yanayohusu maisha binafsi ya mtu yanalindwa na kanuni hii- wanahabari wanaidhinishwa tu kuingilia maisha ya mtu iwapo maisha hayo ya mhusika yameingilia umma.

## 14 Kuingilia majonzi ya watu na mishtuko

1. Kwenye matukio yanayoshirikisha majonzi kwa baadhi ya watu au mambo yanayowashtusha, shughuli za wanahabari kukusanya habari zinapaswa kufanywa kwa moyo wa kuelewa tena kwa busara

2. Katika hospitali, wanahabari wanapaswa kwanza kujitambulisha kisha watafute idhini ya kuwa hapo kutoka kwa afisa msimamizi wa hospitali ile- ili kuingia katika vyumba vya matibabu na wadi, kufuatilia jambo moja au jingine.

## 15 Jinsia na ubaguzi

Wanawake na wanaume wanapaswa kuchukuliwa kwenye mitizamo sawa wakiwa vyanzo vya habari au wahusika kwenye matukio ya habari.

## 16 Uanahabari wa masuala ya fedha

1. Wanahabari wasitumie habari wanazopata kuhusu masuala ya pesa, ambazo wanazipata mapema, kujifaidi wao wenyewe- vilevile hawapaswi kutoa habari hizo kwa marafiki ili pia wajifaidi mapema.

2. Wanahabari wasichapishe au kutangaza habari za hisa kwenye masoko, au dhamana na mambo mengine muhimu kwenye masoko ya hisa hasa namna ambavyo hisa hizo na dhamana zinaendelezwa na wanajua kwamba wao wenyewe au familia zao na marafiki zinahusika, kabla kumwarifu mhariri wa chombo ukweli -kwamba wao ni wahusika kwenye shughuli ile.

3. Wanahabari wasinunue au kuhusika kwa namna yoyote kwenye hisa na dhamana, iwe moja kwa moja au kupitia ma-ajenti wao, au kuhusika kwenye mambo mengine muhimu kwenye masoko iwapo wana lengo la kuchapisha habari kuhusu hisa hizo, siku za usoni.

## 17 Barua kwa mhariri

Mhariri anayetoa nafasi ya kuchapisha barua gazetini kuhusu suala lenye ubishi au linaloibua hamasa si lazima achapishe barua zote zilizopokelewa na chumba cha habari kuhusiana na suala hilo. Mhariri anaweza kuamua kuchapisha tu baadhi ya barua iwe zote au baadhi na sehemu ya kila barua almuradi amepata maudhui ya barua hizo. Hata hivyo, kadri mhariri anapotumia haki yake kufanya hivyo yafaa ajaribu juu chini kuhakikisha kwamba kile kinachapishwa kutoka kwenye barua hizo kinawakilisha pande zote zinazozozana wala sio upande mmoja. Vilevile suala linalozozaniwa lieleweke vyema kupitia barua hizo. Mhariri atatumia busara yake kukomesha mjadala wowote utakaofuata – hasa iwapo hatua yake ya kutoa nafasi ya watu kutuma barua imeanzisha mjadala mpya.

## 18 Kulinda watoto

Taarifa inayohusu watoto walioathiriwa kwenye mikasa ya dhuluma za kimapenzi haitachapishwa au kupeperushwa na wanahabari. Iwapo sio waathiriwa bali ni mashahidi wa dhuluma zile, habari yao vilevile haitachapishwa au kupeperushwa. Ikija kwenye masuala ya kutetea haki za watoto ambayo yana umuhimu mkubwa kwa umma wanahabari wanaweza kutumia majina ya watoto mfano wale ambao wametelekezwa, lakini wanahabari hawatawahoji watoto au kutumia picha zao bila idhini

ya watu wazima wanaowalinda watoto hao. Mahojiano hayo pia yanafaa kuhusu maslahi ya watoto hao. Watoto hawatatafutwa wakiwa shule au tasisi nyingine ya mafunzo ili wahojiwe au kupigwa picha – bila idhini ya wasimamizi wa shule.

Ikiwa njia ya kutii kanuni hii wanahabari wanapaswa kukumbuka visa maalum vya hapa na pale vinavyowahusu watoto wanaopitia maisha magumu au wanaokumbwa na matatizo yanayofaa kuangaziwa

## 19 Waathiriwa wa dhuluma za kijinsia

Vyombo vya habari havitawatambua waathiriwa wa dhuluma za namna yoyote iwe za kimapenzi au jinsia. Vyombo vya habari havitachapisha habari zinazochangia katika kuwezesha wajulikane. Kuchapisha habari kama hizo hakufaidi mwanahabari lolote wala kuufaa umma - hata kwaweza kuchangia katika kuwaongezea madhila na aibu waathiriwa, jamaa zao, familia, marafiki, jamii, na makundi yao ya dini.

## 20 Kutumia picha na majina

Ni hitaji muhimu kwamba vyombo vya habari vinapaswa kuwa angalifu kila vinapotumia picha na majina – vinapaswa kujiepusha na uchapishaji iwapo upo uwezekano wa kuwadhuru watu wanaohusika. Kuzigeuza picha kwa njia inayobadilisha uhalisia kusifanywe katu. Picha zinazoonyesha majonzi, majanga na zile zinazoaibisha na kuendeleza taasubi inayochochea ubaguzi wa kijinsia zafaa kuepukwa.

## 21 Jamaa na marafiki ambao hawajahusika kwenye tukio

Vyombo vya habari vinapaswa kuepuka suala la kuwatambua na kuwashirikisha kwenye visa, jamaa na marafiki wa watu wanaotuhumiwa makosa ya uhalifu hasa iwapo hawakuhusika. Iwapo kuwashirikisha kwenye habari hizo kutawawezesha wanahabari kuboresha viwango vya kuufahamisha umma, kuhakikisha usahihi wa habari zao au uzingatiaji haki basi itafaa wanahabari wawashirikisha jamaa.

## 22 Matendo ya Vurugu

Vyombo vya habari vinapaswa kujiepusha na hali ya kuangazia, kuchapisha na kupeperusha habari zinazohusu vurugu, wizi, ujambazi, matukio ya ugaidi kwa njia inayosifia ushujaa wa wakosaji kama hao na mienendo mingine sawa na hiyo. Kurasa za magazeti zinapaswa kuepuka kutumika  kachapisha makala maalum yanayosifia maovu ya kijamii, hamasisho ya vita na fujo, ukabila, ubaguzi wa rangi na mizozo ya kidini.

## 23 Majukumu ya mhariri

Mhariri atawajibikia mambo yote yanayochapishwa gazetini ikiwemo matangazo ya kibiashara. Iwapo uwajibikaji unafaa kuwaendea watu wengine basi suala hilo lafaa lisemwe mwanzo kabisa.

## 24 Matangazo ya kibiashara

Mhariri hapaswi kuruhusu matangazo ya kibiashara ambayo maudhui yake ni kinyume cha kanuni hizi za utendakazi wa uanahabari nchini Kenya yachapishwe. Kutokana na hayo mhariri atafuata mwongozo wa matangazo ya kibiashara almuradi unakubaliana na mwongozo anaotumia yeye akiwa mhariri chini ya kanuni hizi.

## 25 Matamshi ya chuki

Kuwanukulu watu wanaotoa matamshi yanayowavuruga watu huku wakirejelea makabila yao, jamii zao, makundi yao, rangi yao ya ngozi, na jinsia yao kwafaa kuepukwa na Vyombo vya habari. Matamshi ya kikabila na yanayashiria ubaguzi wa rangi yanafaa kuepukwa. Tathmini ya uangalifu yafaa kufanywa kuihusu jamii inayosemwa vibaya hasa kuhusu namna itaathirika kwa matamshi kama hayo. Vilevile yafaa kutathmini kuhusu namna ambavyo umma unayachukulia matamshi hasa kuhusu yale yanayokubalika na yale yasiyokubalika.

MEDIA COUNCIL OF KENYA

# Kanuni za utendakazi wa uanahabari nchini Kenya

## Jedwali la Pili la Sheria ya Baraza la Habari la 2013

Sheria ya Baraza la Habari la 2013

P.O. Box 43132-00100 Nairobi,
Kenya Tel: + 254 (0) 20 2725032
+ 254 (0) 20 2737058
Cell:+ 254 (0) 727 735252
E. info@mediacouncil.or.ke
Web: www.mediacouncil.or.ke